Toleo 80 - Safar 1445 H / Septemba 2023 M

TOLEO MAALUM

# Jarida la UQAB



# Misimamo ya Kishujaa

بسم الله الرحمن الرحيم

# Tahariri

Tungependa kuwakumbusha wasomaji wetu kuwa tumo ndani ya mwezi wa Safar. Mwezi ulioshehenі matukio makubwa katika historia ya Kiislamu. Moja miongoni mwa matukio hayo ni pamoja na tukio lililojiri Safar Mwaka wa 14 wa Utume. Tukio la Viongozi wa Maquraysh kukongamana katika Dar al-Nadwa. Kongamano ambalo halijawahi kufanyika na ambalo Iblis alishiriki. Lengo likiwa ni kupanga njama ili kumuua mbebaji haki ambaye si mwengine bali ni kipenzi chetu, mwalimu wetu, mtume wetu na Rais wetu wa kwanza wa Serikali yetu ya kwanza ya Kiislamu; Muhamamad ibn Abdullah (saw).

Hakika, katika tukio hilo Iblis aliyelaaniwa na Mwenyezi Mungu (swt), alihudhuria kwa sura ya mwanamume mzee kutoka Najd. Baada ya rai nyingi kutolewa na zote kupingwa na Iblis, hatimaye aliiunga mkono rai ya Abu Jahl Mwenyezi Mungu (swt) amlaani nayo ni kumuua Mtume (saw). Mwenyezi Mungu (swt) alisema:

وَإِذْ يَمْكُرُ بِكَ الَّذِينَ كَفَرُوا لِيُثْبِتُوكَ أَوْ يَقْتُلُوكَ أَوْ يُخْرِجُوكَ ۚ وَيَمْكُرُونَ وَيَمْكُرُ اللَّهُ ۖ وَاللَّهُ خَيْرُ الْمَاكِرِينَ

**“Na walipo kupangia mpango walio kufuru wakufunge, au wakuuwe, au wakutoe. Wakapanga mipango yao, na Mwenyezi Mungu akapanga yake. Na Mwenyezi Mungu ndiye mbora wa mipango.”** [8. Anfal: 30]

Ni muhimu kutambua kwamba viongozi miongoni mwa Maquraysh walikuwa wanasiasa wanaona mbali. Hivyo basi, walitambua kuwa Muhammad lau angelifaulu kuhamia Madinah na kusimamisha Serikali ya Kiislamu naye akiwa Rais wa kwanza kwa msingi wa itikadi (aqeedah) ya Kiislamu ya Kisiasa. Basi, katu hawatokuwa na fursa ya kufurahia ubwana wao uliokuwa umejikita katika ukafiri.

Njama zao hazikufua dafu kwa sababu ikiwa kabla kupiga njama dhidi ya kumuua Mtume (saw), walishindwa kuwazuia Masahaba (ra) kuhamia Madinah. Walitumia mbinu tofauti ikiwemo za kuzitenganisha familia zao (Abu Salamah, mkewe na mwanawe), kuwateka nyara na kuwafunga (Hisham ibn al-’Aas na Ayyash) na kuwapora mali zao (Suhaib ar-Rumi). Hayo yaliwafika Masahaba (ra) na Mtume (saw) katika kipindi cha Miezi ya Muharram na Safar Mwaka wa 14 wa Utume.

Kilichosababisha kupangiwa njama zote hizo ni kwa sababu walikuwa na misimamo thabiti juu ya dini yao. Dini ya Uislamu haitaki watu wa kuyumbayumba wanaopiga hesabu za faida na hasara au wepesi na ugumu wanapotakiwa kumuitikia Mwenyezi Mungu (swt) na Mtume wake (saw). Mwenyezi Mungu (swt) alisema:

يا أَيُّهَا الَّذينَ آمَنُوا استَجيبوا لِلَّهِ وَلِلرَّسولِ إِذا دَعاكُم لِما يُحييكُم ۖ وَاعلَموا أَنَّ اللَّهَ يَحولُ بَينَ المَرءِ وَقَلبِهِ وَأَنَّهُ إِلَيهِ تُحشَرونَ

**“Enyi mlio amini! Muitikieni Mwenyezi Mungu na Mtume anapo kuitieni jambo la kukupeni uzima wa milele. Na jueni kuwa Mwenyezi Mungu huingia kati ya mtu na moyo wake, na kwamba hakika kwake Yeye tu mtakusanywa.”** [8. Al-Anfal: 24]

Na imepokewa kutoka kwa Sufyan bin Abdullah (ra) kwamba Mtume (saw) alisema:

قُلْ: آمَنْت بِاَللَّهِ ثُمَّ اسْتَقِمْ

**“Sema. ‘Namuamini Mwenyezi Mungu na kisha uwe na msimamo.’”** [Muslim].

Kwa kuongezea Mwenyezi Mungu (swt) alisema:

وَالْعَصْرِ.إِنَّ الْإِنسَانَ لَفِي خُسْرٍ.إِلَّا الَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ وَتَوَاصَوْا بِالْحَقِّ وَتَوَاصَوْا بِالصَّبْرِ.

**“Naapa kwa Zama! Hakika binadamu bila ya shaka yumo katika hasara. Ila wale walio amini, na wakatenda mema, na wakausiana kwa haki, na wakausiana kusubiri.”** [103. Al-Asr: 1 -3]

Mtume (saw), Masahaba (ra) na wema waliotanguliwa walikuwa na misimamo juu ya dini yao na kwa sababu hiyo Mwenyezi Mungu (swt) akawaridhia dini yao na kuhakikisha wako juu ya ukafiri na makafiri. Leo hali yetu Waislamu iko tofauti na walio tutangulia. Kila upande umesheni ufisadi kuanzia

***Endelea... UK 3***

bara mpaka baharini. Uchafu umetapakaa kuanzia huko Magharibi wanakojidai eti ndio ngome ya ustaarabu hadi huku nchini mwetu ambako sio lolote bali ni mashamba ya wakoloni Wamagharibi.

Nchi zetu zipo kwa ajili ya kuporwa rasilimali zake, watu wetu wakifanyishwa kazi za utumwa kwa vijipesa duni ili kuhakikisha wanaendelea kupumua ili wahakikishe muendelezo wa ufyonzaji wa madini, mali ghafi nyeti, ardhi zenye rutuba, mafuta, gesi n.k. Tuko katika hali hii kuanzia pale tulipojitenga na Qur'an na Sunnah. Fauka ya hayo, tukawaruhusu makhaini wakiongozwa na Mustafa Kamal kuivunja Serikali yetu ya Kiislamu huko mjini Istanbul mnamo 28 Rajab 1342 H sawa na 3 Machi 1924 M. Hadi sasa ni zaidi ya miaka mia moja na tatu (103), bado tunaangamia na kuteketea ndani ya moto wa mfumo wa kirasilimali ambao chimbuko lake ni usekula (ilmaniyah) – kutenganisha dini na maisha au serikali.

Baadhi yetu tukiwa tumeridhika na Uislamu Poa, aina ya Uislamu wa kujitia hamnazo juu ya Siasa ya Kiislamu. Kwa maana nyingine tumekuwa Waislamu tuliosalimu amri mbele ya ukafiri na makafiri na kuwaacha watutawale watakavyo kwa kutumia nidhamu ya kidemokrasia au kifalme n.k. Hivyo basi, Muislamu kutoona haya wala vibaya kushiriki na kutoa mchango katika vyama vya kisiasa za kidemokrasia na hata ikibidi kujitoa uhai eti anatetea nidhamu ya kiutawala ya kidemokrasia! Kiuhalisia ni kupitia demokrasia ndio mwanadamu hupata uhuru wa kuabudu (kuabudu pesa, watu, wanyama n.k), uhuru wa kumiliki (kutoa na kuchukua hongo, mikopo ya riba, kuwapora watu mali zao kupitia ushuru, kufanya ukahaba, kamare n.k), uhuru wa kibinafsi (kuwa shoga, msagaji, kuvaa utakavyo n.k) na uhuru wa maoni (kuwatusi na kuwavunjia watu heshima na matukufu yao ikiwemo Mtume (saw) n.k).

Kukosa kuwa na msimamo ndio kumetupelekea kutumbukia katika fedheha na ukandamizaji. Twashuhudia watu wamevuka mipaka kuwashinda wanyama, familia zimevunjika, elimu inayozalisha wajinga wengi, siasa na vyeo vya kisiasa vikibuniwa na kukaliwa na wajinga na waliobobea katika ufisadi; uchumi uliosimama juu ya msingi wa riba na utozaji ushuru na mengine mengi maovu. Majonzi na vilio vimesheheni duniani kote. Kila anayenyoosha mkono kutafuta msaada, unatafunwa na papa wa kirasilimali waliojivika ngozi za kondoo ilhali ni mbwa mwitu wanaoendelea kunenepa kwa kunywa damu za kondoo walioko zizini!

Enyi wasomaji, hamuoni kuwa twastahiki kuwa na ngao na mlinzi wa kweli? Je, twatarajia ulinzi na usalama kutoka kwa Umoja wa Mataifa (UN), Amerika, Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Muungano wa Ulaya (EU), Uchina au Urusi? Kiuhalisia hawa ndio asili ya matatizo yetu, wao ndio wa mwanzo katika kuchochea ukosefu wa utulivu ulimwenguni kupitia sera na sheria zao walizozitunga ambazo chimbuko lake ni akili zao finyu zisizodiriki litakalojiri sekunde moja ijayo!

Hii ni fursa muafaka kuchukua msimamo thabiti, kama ile iliyochukuliwa na Mtume (saw), Masahaba (ra) na wema waliotangulia kabla yetu sisi. Misimamo yenye kuthibitisha kuwa sisi ni watumwa wa Mwenyezi Mungu (swt) na ubwana ni kwa Shari'ah yake. Hakika, ili kufikia hilo ni mpaka sisi Waislamu tufanye kazi ya kurudisha maisha ya Kiislamu kupitia kusimamisha tena Serikali ya Kiislamu ya Khilafah kwa njia ya Utume. Kazi hii tayari inafanywa na Chama cha Kisiasa cha Kiislamu cha Hizb ut Tahrir, na kinaendelea kuwa safu ya mbele katika ulinganizi wa kurudisha tena maisha ya Kiislamu. Hata hivyo, hili ni jukumu la kila Muislamu popote alipo kushiriki kikamilifu kwa kadri ya uwezo wake wa mwisho kabisa. Hivyo basi ni jukumu letu sote Waislamu kushirikiana kwa pamoja pasina kuzingatia tofauti zetu za kikabila, kiuchumi, kimadh-habi ili tuweze kuungana chini ya Itikadi

***Endelea... UK 4***

ya Kiislamu ya Kisiasa tuweze kuokolewa na dhiki hizi. Hatimaye tuweze kuwa juu kwa kupata utukufu na uongozi duniani kwa kuwa chini ya Dola Moja ya Khilafah, Mtawala Mmoja ambaye ni Khalifah na Ummah Mmoja ambao ni Ummah wa Kiislamu. Mwenyezi Mungu (swt) alisema:

وَلَن يَجعَلَ اللَّهُ لِلكافِرينَ عَلَى المُؤمِنينَ سَبيلًا

**“Na asilani kamwe Mwenyezi Mungu hatawapa makafiri njia (mamlaka/utawala/uongozi/madaraka) ya kuwashinda Waumini.”** [4. An-Nisa’: 141]

Enyi wasomaji, hamuja choka kubahatisha kuwekeza juhudi na rasilimali katika vyama vya kisiasa vya kidemokrasia? Tukio la Waamerika kuvamia bunge lao (Congress) mnamo Jumatano, 6 Januari 2021, halijawapa uthibitisho kuwa mungu anayeitwa Demokrasia amefeli kabisa kutatua matatizo yanayoikumba dunia kwa ujumla? Hilo ni dhihirisho kuwa wanadamu wamekata tamaa na nidhamu ya kiutawala ya kidemokrasia na mfumo wake wa kirasilimali wa kisekula. Na njia pekee iliyobakia ni kurudi kwa Muumba wa ulimwengu, mwanadamu na uhai naye si mwengine isipokuwa ni Mwenyezi Mungu (swt). Yeye pekee ndiye anayestahiki kutupangilia namna ya kuishi na kutatua matatizo yetu kama wanadamu.

Mifumo ya Urasilimali, Ukomunisti na Ujamaa imefeli na kila mmoja wetu anashuhudia suluhisho za viraka. Suluhisho ambazo huzalisha matatizo mapya kila uchao. Hakika njia pekee iliyobakia ni kuurudia mfumo wa Uislamu kwa msingi wake wa Itikadi ya Kiislamu ya Kisiasa. Kupitia Itikadi ya Kiislamu ya Kisiasa ndio chimbuko la Serikali ya Kiislamu ya Khilafah. Khilafah ambayo ilitawala zaidi ya karne kumi na tatu (13) na kueneza amani, usalama, utulivu na ustawi kwa wanadamu jumla. Historia iko na imesheni ushahidi wa kupitiliza juu ya mafanikio ya Serikali ya Kiislamu ya Khilafah kabla kuvunjwa kwake na maadui wa Uislamu na Waislamu kwa kushirikiana na makhaini miongoni mwa safu za Waislamu.

Kazi ya ulinganizi wa kurudisha maisha ya Kiislamu kupitia kusimamisha Serikali ya Kiislamu kwa njia ya Utume hujumuisha mbinu za kifikra na mivutano ya kisiasa ndani ya Ummah. Katu! Hawezi kufaulu katika kazi hii yeyote yule ambaye hana msimamo juu ya Dini ya Uislamu kwa kujifunga kikamilifu na Itikadi ya Kiislamu ya Kisiasa. Kwa sababu siasa ya Kiislamu ni kuwasimamia watu mambo yao kwa kuirudia Itikadi ya Kiislamu ya Kisiasa kwa mtazamo wa kipimo cha Halali na Haramu katika vitendo vya mwanadamu. Hakuna budi wanaume, wanawake na mabarobaro kushirikiana na kuwa na kuchukua misimamo kwa kuwaiga wema waliotangulia katika kufanya kazi hii adhimu. Kazi iliyowapa hadhi za juu na majina yao kunakiliwa katika historia kwa kuwa na misimamo thabiti.  Kurasa zinazofuata zitadondoa baadhi ya matukio na misimamo ya wema waliotangulia; ili wewe msomaji uweze kuzinduka kutoka usingini na kuchukua hatua na misimamo itakayobadilisha mwelekeo wa hali ya kutamausha iliyoko sasa.

Amka! Mustakbali wa kubadilisha hali ya sasa iko mikononi mwako. Jiamini waweza na songa mbele, kunyamaza kwako ndio chanzo cha dhalimu kuendelea kutukandamiza na uovu kuenea kila nyanja ya maisha. Babu yako, babako, wewe mwenyewe na wanao pamoja nasi tutaishi kwa majonzi mpaka lini? Kila kukicha afadhali jana, au afadhali dhalimu yule aliyeondoka mamlakani. Kila kukicha kitanzi kinakazwa huoni kuwa mwisho kitatuua? Au wadhania kunyamaza kimya na kutochukua hatua na  misimamo ndio suluhisho? Zinduka, ukisema haki hutokufa mapema na kunyamaza kimya hutoishi milele! Wakati ndio huu, patiliza fursa ya kujiunga ufanyekazi ya ulinganizi wa Khilafah popote ulipo hususan ulimwengu wa Waislamu.

**Mifano ya misimamo ya kishujaa tunayowasilisha hapa imenukuliwa kutoka katika mtiririko wa mada kwa kichwa cha* **‘Misimamo ya Kishujaa’ iliyowasilishwa na Sheikh Abu Nizar Ash-Shami na kupeperushwa katika Ummah Voice Podcast.**

*Utangulizi wa Mada:

*Maisha yetu ni mkusanyiko wa misimamo tuliochukua. Misimamo hii ndio itakayoamua hadhi na thamani yetu mbele ya Mwenyezi Mungu (swt) Siku ya Hukumu. Misimamo ya kishujaa, iliyobadilisha mkondo wa historia, ikazalisha matukio, na kuwashawishi wote walioishuhudia au kuisikia. Misimamo ya kishujaa, tunayoitaja ilhali tunaishi zama ambapo misimamo tunayoiona ni ile ya kufedhehesha na aibu. Misimamo ya kishujaa, tunaitaja ambayo mashujaa wake wametajwa katika Qur’an, na kurasa za Seerah, zama za Ummah wetu na historia ya hivi majuzi imejaa ndani yake. Misimamo ya kishujaa, ambayo tunaitaja ili kuweza kujifunza kutokana nayo. Tunaitaja ili kupata mshawasha wa utukufu, matumaini na kutarajia heri kutoka kwa Mwenyezi Mungu (swt), na kuthitibisha kwamba Ummah wetu, kwa idhini ya Mwenyezi Mungu (swt) una uwezo wa kurudisha tena misimamo yenye hadhi ambayo itaijaza dunia uadilifu na wepesi baada ya kujazwa dhuluma na ukatili.*

بسم الله الرحمن الرحيم

# Iyas Bin Muadh (ra)
# Kuwapelekea Vijana Fursa za Da’wah

Katika misimamo ya kishujaa ni ile ambapo ushujaa upo katika kupatiliza fursa – kupatiliza fursa adhimu, ambayo ndani yake upo ushindi wa Uislamu na kufanikiwa kwa haki na uadilifu. Hivi ndivyo shujaa wa hadithi yetu ya leo alivyofanya: Sayyiduna Iyas bin Mu'adh (ra).

Katika kipindi cha mwanzo wa Uislamu, kipindi cha Makkah, Iyas bin Mu'adh (ra) alikuwa anatoka Madinah kutoka Bani Abd Al-Ashhal kutoka kabila la Aws. Kiongozi wao Anas bin Rafi', alikuja na wawakilishi kutoka Aws hadi Makkah ili kukutana na Makafiri Maquraysh ili Makafiri Maquraysh waweze kuwa washirika nao dhidi ya Khazraj ndani ya Madinah. Hapa, kijana mdogo, Iyas bin Mu'adh (ra) naye pia alikuja, na walipofika Makkah, Mtume (saw) akawajia. Yeye (saw) akajuwa kilichowaleta: ushirika wa kisiasa dhidi ya Khazraj. Kwa hiyo, yeye (saw) akawaambia: “Nisiwaelekeze kwa lile ambalo ni bora zaidi kuliko hili?” Wakasema: “Na nilipi hilo?” Yeye (saw) akasema kwamba Yeye ni Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw), akawalingania kuingia katika Uislamu na kuwasomea Qur’an. Kisha kiongozi wa wawakilishi, Anas bin Rafi', akasimama na kusema: “Hatuna haja na wewe wala hatuutaki huu ujumbe.” Huyo kijana, Iyas bin Mu'adh (ra), alisikia hilo na alikuwa mdogo kabisa katika watu wake. Hali hiyo ilitaka kuchukua msimamo. Kwa hiyo, alisimama miongoni mwa watu wake – kabila lake – na akasema: “Enyi watu, kwa jina la Mwenyezi Mungu (swt), anachotulingania Muhammad (saw) ni bora zaidi kuliko tuliyoyafuata, kwa nini tusimfuate?”
Kiongozi wao, Anas bin Rafi' aliposikia hivyo alichukua mchanga mkononi mwake na kumpiga nao usoni kisha wakaanza kupigana miongoni mwao. Kisha, ushirika wao haukufaulu na wakarudi Madinah bila kufanikiwa na lolote.

Walifika Madinah na kisha vita vya Bu’ath vikaanza. Ilikuwa ni siku chache tu baada yake ndipo walipo mpata Iyas bin Mu'adh (ra) akipumua pumzi zake za mwisho kitandani. Hata hivyo, lakustaajabisha walimsikia akisema: “Subhanallah wa Alhamduillah wa la ilaha illah Allah wa Allahu Akbar.” Alikuwa anafanya Tahleel na Tasbeeh, na kufariki akiwa Muislamu.
Yeye (ra) alikuwa ni mmoja katika Ansar wa mwanzo waliomnusuru Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw) kwa msimamo mmoja aliouchukua wakati wa mkutano mmoja tu wakiwa Naye. Ndugu zangu, twaona tofauti katika maamiliano na misimamo inayochukuliwa katika kuitikia unaposikia Da’wah. Mwenyezi Mungu (swt) asema: “Hakika, juhudi zenu ziko tofauti.” “Ama kwa yule anayetoa na kumuogopa Mwenyezi Mungu. Na kuamini.” Na kuna yule pia ambaye “anaficha na kujiona kuwa amejitosheleza. Na anakana.” Iyas bin Mu'adh (ra) aliona fursa na kuunusuru Uislamu.

Lau ushirikiano huu ungelifaulu baina ya Aws na Maquraysh, Hijra ya Mtume (saw) kwenda Madinah ingelisambaratika na Da’wah yake isingepiga hatua kwa urahisi kama ilivyofanyika miongoni mwa Aws na Khazraj. Nani aliyekuwa shujaa katika hilo? Alikuwa ni kijana mdogo! Hivyo basi, ndugu zangu, maisha yetu ni mkusanyiko wa fursa. Kwa hiyo, je unachukua misimamo thabiti juu ya haki? Kwa masikitiko, ndugu zangu, wakati mwingine wa mwanzo kukuekea kizuizi na kukuzuia katika Da’wah na kutokuruhusu kuchukua misimamo ya kishujaa inayonusuru haki, ni wanafamilia au watu wako wa karibu. Kwa hiyo, utasalimu amri kwa hali iliyoko hivi sasa na kuiacha haki ili kuifurahisha familia yako na watu walio kuzunguka? La. Ibn Al-Qayyim (ra) asema: “Kuwa upande wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake hata kama watu wote wako upande mwingine.”

Fursa zinazopatikana katika maisha yetu na zinazohitaji misimamo ya kishujaa kuchukuliwa ni nyingi. Ilhali umo ndani ya teksi, waweza kumsikia abiria akielezea kukasirishwa na Mwenyezi Mungu. Ilhali ukiwa chuoni, unaweza kusikia uhadhiri au maneno kutoka kwa mhadhiri ambayo yanautusi Uislamu na kuulaumu kwa ugaidi. Ndugu zako wanaweza kukualika ujiunge na Da’wah ya Kiislamu ambapo utajifunza namna ya kuunusuru Uislamu na kufanyakazi ya kusimamisha Dola yake. Kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, unapokuwa katika hali zote hizi, chukua msimamo ambao utamridhisha Mwenyezi Mungu na kuunusuru Uislamu na watu wake na chukua msimamo ambao utakupa tunu na kukipa nuru kitabu cha matendo yako kwa Mwenyezi Mungu (swt) kabla kukutana Naye (swt) ukiwa miongoni mwa wanaojutia.

بسم الله الرحمن الرحيم

# Abu Dhar Al-Ghifari (ra)

Je, wamjua Afeef Al-Kindi ni nani? Natarajia wengi wenu hamumjui. Nani miongoni mwetu asiyemjua Abu Dharr Al-Ghifari (ra)? Tofauti baina ya hao wawili, kaka na dada zangu – wote waliishi wakati mmoja na waliona matukio sawa lakini msimamo ambao kila mmoja alichukua ndio tofauti baina ya ushujaa na kinyume chake.

Afeef Al-Kindi alikuja Makkah kufanya biashara na Al-Abbas na wakati anafanya biashara, aliona tukio la kushangaza. Alisema, "Nilimuona mwanamume akitoka nyumbani kwake kwa ajili ya kusali…" Kwa maana Nabii (saw). "Abbas, huyu ni nani?" Yule ni mpwa wangu." Kisha Sayyida Khadija (ra) akasimama nyuma yake na Ali (ra) karibu naye. Afeef alisema: "Anafanya nini?" Abbas alisema: "Anasali." Anasema yeye ni Muislamu ametumwa na Muumba wa Mbingu na Ardhi na kwamba atawakomboa Warumi na Wafursi." Fitra ya Afeef Al-Kindi ikaanza kusonga. Al-Abbas akapatiliza fursa: "Je, nizungumze naye kukuhusu? "Je, nizungumze naye kwa ajili yako" akimaanisha akutane naye? Kukutana naye? Akimaanisha kumuamini au la? Mwanamume ambaye anakwenda kinyume na sheria za watu wake – gharama ya kufanya hivyo inaweza kuwa chungu mno. Afeef alifanya maamuzi mabaya kabisa katika uhai wake na kuchukua msimamo ambao aliujutia katika kipindi cha uhai wake wote. Mtazamo wake ni kama kusema: "La, Abbas, tubakie na biashara yetu." Kutokana na msimamo aliouchukua Afeef bin Qays hapa, alirudi nchini kwake na kuingia katika Uislamu miaka 20 baadaye. Miaka 20 baadaye, wakati kila mtu ashaukumbatia Uislamu katika mwaka wa wawakilishi mnamo mwaka wa 9 baada ya Hijria. Kila mtu alikuwa na furaha na bashasha isipokuwa Afeef aliyekuwa akilia. "Ni nini kinachokuliza, Afeef? Ni siku ambayo mtu yeyote hatakiwi kuwa na majonzi." Alisema: "Nalia kwa sababu ningelikuwa wa nne katika Uislamu." Nambari 4! Angelikuwa Mislamu wa nne.

Alikosa nini? Kwa jina la Mwenyezi Mungu (swt), alikosa heri nyingi. Alikosa kuwa katika safu za mbele. Alikosa kuwasaidia Masahaba katika kusimamisha Dola ya Kiislamu. Alikosa Badr, Uhud, Khandaq na mengine mengi matukufu. Wakati huo huo, ndugu zangu, Abu Dharr alikuwa huko Ghifar ambacho kilikuwa kijiji cha mbali. Alimsikia Mtume (saw) na ulinganizi wa Uislamu. Pia alisikia vyombo vya habari vyenye kupotosha ambavyo viliwatishia watu kutomfuata Yeye (saw). Walidai kuwa ni "Mpigaji raml," "Mshairi," "Mchawi," "Mwendazimu," "Visa vya Kale," nk; na kwamba yeyote anayeulizia kumuhusu atapigwa. Alimtuma nduguye kukusanya taarifa zaidi lakini hakuridhika. Kwa hiyo, akaamua kuchukua hatua mwenyewe na kusafiri kutoka Ghifar mpaka Makkah pekee, akijua hatari ya kumuuliza mtu huyu ambaye ni marufuku kumuulizia. Alikaa siku na mahitaji yake yakamuishia. Akawa anakula na kunywa kutoka kwa Zamzam mpaka tumbo lake likaingia ndani na ngozi yake kubadilika. Sayyiduna Ali (ra) alikutana naye na kumchukua kama mgeni kwa siku 3 kisha Ali (ra) akamuuliza: "Haujafika muda mtu kujua yuko upande gani?" Alijibu: "Naam." Sasa akaamua kuchangamka na kuchukua hatua kwa kutangaza nia yake. Alisema: "Nielekeze alipo Muhammad (saw)." Ni kiwango gani, kaka na dada zangu kinachohitajika ili dunia iweze kuelekezwa kwa Muhammad (saw). Abu Dharr (ra) aliingia na kukutana na Mtume (saw). Alifurahi na kutoa salamu wa mwanzo. Alisema: "Assalamu Alaika Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw)." "Watoka wapi." "Kutoka Ghifar." Nabii (saw) alisema: "SubhanAllah! Kutoka Ghifar?" Ardhi maarufu ya uhalifu, mauaji na waporaji wa barabara kuu. Umeacha yote hayo na kuja huku? Umeishinda nafsi yako na propaganda zote hizi na kukutana na Mtume (saw)? Mtume (saw) akamlingania Uislamu, na papo hapo akasilimu. "Waniamrisha nini, Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw)?" Mazoea ya Mtume (saw) kwa kila Muislamu mpya, hata kama Uislamu wao ni wa dakika moja: "Nenda ukawalinganie watu wako. Ukiona nimepata ushindi, walete kwangu." Alisema: "La, Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw). Kwa jina la Mwenyezi Mungu, nitautangaza wazi Uislamu wangu kwa sauti baina yao."

Kwa hiyo, Abu Dharr (ra) alitangaza wazi Shahadah na alikuwa mtu wa mwanzo kufanya hivyo mbele za viongozi wa Maquraysh. Kwa hiyo, walimpiga mpaka akawa mwekundu kwa damu. Aliokolewa na Al-Abbas na kisha kurudi kwa watu wake. Mtume (saw) hakumuona tena Abu Dharr (ra) kwa miaka 14. Alikuja na makabila 2: Ghifar yote ilikuwa Waislamu na pia Banu Aslam. Mtume (saw) alifurahishwa na hilo na akawaombea Du'a na kumuombea Du'a Abu Dharr (ra), akisema: "Dunia haibebi, wala mbingu hazimfuniki

***Endelea... UK 7***

mwanamume mkweli na muaminifu zaidi ya Abu Dharr (ra).” “Mwenyezi Mungu (swt) amhurumie Abu Dharr (ra)! Anatembea pekee, atakufa pekee na atafufuliwa pekee Siku ya Hukumu.”

Kaka na dada zangu, tupate ushauri kutoka katika moyo kama wa Abu Dharr (ra) na tusiwe kama wa Afeef bin Qays. Tupatilize na tusicheleweshe kujiunga na safu za wabebaji Da’wah, uhai unakatika mara moja na Dunia inakutokomeza mbali na njia ya Mwenyezi Mungu (swt). Usijiwekee vikwazo baina yako na Da’wah kama wanavyotaka watawala leo iwe. “Da’wah itakutia matatani!” “Wabebaji Da’wah wote ni wafisadi!” “Jihurumie!” Vivunje vikwazo vyote hivyo ambavyo vinakuweka mbali na Da’wah kama alivyofanya Abu Dharr (ra). Alizikana propaganda potofu na kwenda mwenyewe kujisikizia kutoka kwa wabebaji Da’wah moja kwa moja. Tunapata funzo kutoka kwa Abu Dharr (ra) kuhusu utukufu wa kuwa wa mwanzo na wa mbele kwenye macho ya Mwenyezi Mungu. “Na wa mwanzo miongoni mwa Muhajireen na Ansar na waliowafuata katika heri - Mwenyezi Mungu amewaridhia.” Abu Dharr (ra) alikuwa akikutana na Masahaba na akisema: “Nilikuwa wa nne katika Uislamu.” Mimi ni nambari 4. Ni katika wa mwanzo. Leo, kaka zangu idadi kubwa ya Hukm za Uislamu hazifanyiwi kazi. Maadui wa Uislamu wanatapakaa duniani kote. Kwa jina la Mwenyezi Mungu (swt), hawako sawa mbele ya macho ya Mwenyezi Mungu (swt): kijana ambaye amekwenda mbio kujiunga na safu za ubebaji Da’wah na akasoma na kutoa juhudi yake yote maishani katika kuilinda Dini yake, na mtu ambaye anayeishi kwa raha anayejijali mwenyewe na usalama wake na akawasubiri wengine kuinusuru [Dini], kwa wengine kufanyakazi ya Da’wah, na wengine kubadilisha hali iliyoko. “Hawako sawa miongoni mwenu wale ambao walitumia kabla kukombolewa [Makkah] na waliopigana [na waliofanya hivyo baadaye]. Wao wana cheo kuwashinda wale waliotumia baadaye na kupigana.”



# Nusaybah bint Ka'b Al-Ansaariyyah (ra) (Umm 'Amara) – Mwanamke Mujahid

Wanapotajwa mashujaa, akili aghalabu hufikiria wanaume. Ukweli ni kuwa, ndugu zangu, shujaa wetu wa leo hakuwacha msimamo wake wa kishujaa pasina kurekodi jina lake miongoni pamoja na ya wanaume. Bali, alishiriki katika misimamo ambayo wanaume waliikimbia. Nusaybah bint Ka'b Al-Ansariyah - Umm 'Amara (ra) alishiriki katika kumpa ahadi ya utiifu Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw) katika Bay'ah ya Aqaba. Alikula kiapo cha Ridwan kwake (saw). Alishiriki katika Uhud, Hudaibiya, na Yamama na alipigana Jihad, akapoteza mkono wake na kufanikiwa katika mambo makubwa. Leo msimamo wa kishujaa wa mwanamke huyu ulikuwa katika Uhud wakati wa janga la Uhud ambapo Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw) alikuwa amezungukwa, wengi katika waliomzunguka wamekimbia na mishale na mashambulizi yalikuwa yanamuelekea. Walikuwa wanamuangalia kisha wanakimbia. Nusaybah (ra) alikuwa amekuja vitani, lakini dori yake ilikuwa sio kupigana. Dori yake ilikuwa ni kuwapa maji ya kunywa wanajeshi. Hata hivyo, alipoona janga linakuwa kubwa kwa Mtume (saw), alichukua msimamo wa kipekee. Aliwacha kila kitu, akawachukua wanawe wawili wanaume na kukimbia nao [kwa Mtume (saw)]. Alisema (ra): "Nilimuona Mtume (saw) huko Uhud na yeye (saw) alikuwa amezungukwa na watu wachache waliobakia naye waliokuwa kama takribani 10. Kwa hiyo, nikawachukua wanangu wavulana na mume wangu, na tukasonga mbele kumlinda Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw)."

Alikwenda kumlinda Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw) akiwa na mumewe na wanawe wawili: Abdullah na Habeeb. Alisimama mbele ya Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw) bila silaha au ngao, lakini alikuwa anamlinda Mtume (saw) kwa mwili wake. Mtume (saw) aliangalia na kuona mwanamume akikimbia lakini alikuwa na ngao. Kwa hiyo, Yeye (saw) alimwambia: "Iangushe kwa ajili ya atakayeitumia kupigana." Kwa hiyo, Nusaybah (ra) akaichukua na kuitumia kumlinda Nabii (saw). Ibn Qamiah akapigana naye alipojaribu kumfikia Nabii (saw) kwa hiyo akasimama mbele yake bila silaha mkononi, kama ambaye alikuwa amejiandaa kwa lolote litakalo kuwa. Alijaribu kwenda upande wa kulia, akamzuia. Na alipojaribu kwenda kushoto, akamzuia, hivyo kumzuia kutomfikia Mtume (saw). Kwa hiyo, alimpiga begani mwake mpaka akaanza kutokwa na damu. Kisha alisonga mbele akimuacha nyuma na kukabiliana na Mus'ab bin 'Umayr.

Hapa ndugu zangu, yeye (ra) na watoto wake walikuwa mbele ya macho ya Mtume (saw). Yeye (saw) alimuangalia na kusema: "Nani ana uwezo wa kufanya unayo yafanya Ewe Umm 'Amara?" Kisha (saw) aliangalia jeraha lake, watoto wake na mumewe, kisha akasema: "Ewe Mwenyezi Mungu wafanye kuwa ni wandani wangu huko Jannah." Hili ndugu zangu, ndio medali ya kilele cha tunu inayopokewa na mashujaa. Kwa hiyo, akasema: "Kwa jina la Mwenyezi Mungu, hakuna linalonifika Duniani linanishtua." Msimamo wa kishujaa mkubwa kutoka kwa mwanamke bora, ndugu zangu, twajifunza kuhusu Da'wah, Jihad na dori ya kisiasa ya mwanamke. Twajifunza dori ya mwanamke katika kuunusuru Uislamu na watu wake na kushiriki pamoja na wanaume katika hali ngumu na misheni zilizojaa mashaka. Ndugu zangu, mwanamke anabeba Da'wah kama mwanamume. Mwanamke anabeba Da'wah, ana wanyanyua wengine, ana shikwa, anatoa Bay'ah na kujitoa muhanga. Tusisahau kwamba shahidi wa kwanza katika Uislamu ni mwanamke. Hususan, Muislamu wa kwanza baada ya Mtume (saw) alikuwa ni Sayyida Khadeejah (ra).

Twajifunza kutoka msimamo huu wa kishujaa kuhusu malezi ya watoto na familia nzima katika njia ambayo inaunusuru Uislamu. Mtoto wake, Habeeb, aliteswa na kukatwa vipande vipande na Musaylama Al-Kadhab aliyemtaka aritadi lakini hakuweza. Na mwanawe, Abdullah, alilipiza kisasi cha kakake kwa kumuua Musaylama Al-Kadhab.

Ndugu zangu, twajifunza kutokamana na familia hii ya waumini kujituma na sio kupatiliza udhaifu katika kuinusuru Dini. Na tusiseme, "lakini mimi ni mwanamke," au "Nimechoka," au "Mimi ni masikini" na kuendelea. Toa mchango wako kwa kadri ya uwezo wako wa mwisho na Mwenyezi Mungu (swt) atakupa nguvu za ajabu.

Enyi wanawake Waislamu, mnaokabiliwa na kampeni ya kimataifa leo ambayo kwamba inalenga kumuangamiza mwanamke, kuiangamiza familia, kuangamiza malezi ya watoto, kuangamiza vijana na inalenga kuipoteza dira familia ambayo Mwenyezi Mungu (swt) anataka iwe jiwe katika ngome ya Uislamu. Tunawataka muwalee watoto wenu waje wainusuru Dini na kufurusha mawimbi yote ya sumu. Watoto wenu watakuwa salama lakini sio kupitia kuwakumbatia, bali kupitia kuwaandaa kuikumbatia Da'wah hii ambayo Umm 'Amara alituonyesha kwa kupitia msimamo wa kishujaa wa kipekee katika kuinusuru. Waleeni watoto wenu waulinde Uislamu ili Dua ya Nabii (saw) kuhusiana na Umm 'Amara itujumuishe sote: "Ewe Mwenyezi Mungu wafanye kuwa ni wandani wangu huko Jannah."

# Abdullah Bin Unays (ra)
# Jeshi la Mwanamume Mmoja

Baadhi ya misimamo ina shahada kama sifa kuu. Misimamo ambayo inaipa kipaumbele maslahi ya Da'wah na Dini kuliko yale ya kibinafsi, na iko makini kuulinda Uislamu dhidi ya hatari kuliko hata nafsi yake.

Baada ya Uhud, ndugu zangu, na hususan mnamo mwaka wa 4 baada ya Hijra, habari mbaya zilimfikia Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw). “Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu, Banu Asad wanakusanyika ili kukupiga vita,” “Kabila fulani na fulani wanajiandaa kukushambulia nk.” Makabila yote ya Kijahiliya sasa wanakusanyana ili kuishambulia Madinah na kuuangamiza Uislamu ndani yake. Na katika habari hatari zaidi zilizofika ni zile za Hudhayl. Hudhayl, ndugu zangu, ni koo za wapiganaji ambao wanahesabika kwa mamia. “Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu, Hudahyl inajiandaa kuja upande uliko.” Mtume (saw), ndugu zangu, aliziangalia kwa makini nyuso za Masahaba. Afanye nini? Hawezi tu kuyatuma majeshi na kuyaeneza kila mahali. Kwa hiyo akachagua shujaa – mwanamume mmoja kufanya namna majeshi yanavyofanya.

Yeye (saw) alimwambia Abdullah bin Unays (ra): Hudhayl wanakusanyika kupigana nasi. Nataka wewe uende kwao, kutana na kamanda wao mkuu, Khalid bin Sufyan Al-Hudhali, muue kisha rudi kwangu. Abdullah bin Unays (ra), ndugu zangu hakumuuliza Mtume (saw): “Wanituma na nani pamoja nami?” “Itawezekanaje niwe peke yangu?” Hakufikiria kuhusu usalama wake katu. Aliomba jambo moja tu: “Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu, hebu nielezee yukoje.” Hilo tu basi. Yeye (saw) alisema: “Ukikutana naye, atakukumbusha kuhusu Shetani. Na ishara moja baina yako na mimi ni kwamba utasisimkwa na nywele.” Akasema: “Siogopi Ewe Nabii wa Mwenyezi Mungu ukinituma mimi.” Yeye (saw) alisema: “Sio chochote bali ni ishara kati yangu na wewe.” Hilo lilikuwa latosheleza kwa Abdullah bin Unays na kukubali misheni ya kukutana na maadui ilhali uwezo wa kurudi salama ni asilimia 0. Abdullah bin Unays (ra) aliondoka na kuwasili Hudhayl. Akafanya ujasusi wa eneo na akaona majeshi, vikosi, safu, silaha na mafunzo, mpaka macho yake yakakutana na Khalid Al-Hudhali. Alisema: “Ilikuwa kama ambaye anaifanya Ardhi ipasuke;” alikuwa amezungukwa na maafisa na bendera kutoka kila upande. Alisema: “Kisha nikahisi kusisimkwa ambako Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw) alikuwa amenitajia.” Kwa hiyo, akasonga mbele kuelekea aliko kuwa lakini akatambua kuwa muda wa Sala ya Adhuhur unakaribia kuisha. Akasema: “Niliogopa kwamba lau nitachelewa (kusali) na kupigana naye (Khalid), basi ningeliikosa Sala.” Kwa hiyo, alisali ilhali yuko juu ya farasi wake kwa kutumia ishara.

Ijtihad hii kisha baadaye ikaja kuwa ndio Sunnah inayojulikana kama Salat al-Talib wal- atloob (Sala ya mwenye kufukuza na kufukuzwa) Tizama tunu iliyopewa shujaa huyu! Akasonga mbele, Abdullah (ra) and Khalid Al-Hudhali walikutana. Khalid akamwambia: “Wewe ni nani?” Akasema: “Mwanamume muarabu niliyesikia kuwa munajikusanya dhidi ya Muhammad, kwa hiyo nimekuja kujiunga nanyi.” Kisha akajitia hamnazo kwa muda ili kumpotezea, mpaka walipokuwa katika eneo la mafichoni na wakawa peke yao kisha akamuua. Alimwambia: “Chukua hili kutoka kwa pigo la muumini aliyejifunga na Dini ya Mtume Muhammad (saw). Na lau Mtume (saw) alikuwa ameyaelekeza macho yake kwa Kafiri, ningelikuwa wa kwanza kwa mazungumzo na vitendo.” Kisha yeye (ra) akaondoka eneo la mafichoni kimya kimya pasina kuonekana na yeyote, kisha akakimbia kwa Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw) ili kumpa taarifa nzuri. Kabla hajasema kitu chochote, Nabii wetu (saw) alimuona na kusema: “Uso uliofaulu, Ewe Abdullah.” Kisha, Yeye (saw) akampa bakora yake na kusema: “Hii ni ishara kati yangu na wewe Siku ya Hukumu.”

Ndugu zangu, Nabii wetu (saw) hayuko nasi leo. Hata hivyo, utukufu wa Nabii (saw) upo katika ujumbe na Shari'ah Yake. Na leo, majeshi yanakusanyika na kushambulia Shari'ah ya Uislamu, mashirika ya habari yanabuniwa ili kuwasilisha kimakosa na kuuharibu Uislamu na kuwaweka mbali Waislamu na kutoutekeleza. Kwa hiyo nani atakuwa kama Abdullah bin Unays? Je, utakuwa kama huyu shujaa ambaye anakwenda pekee dhidi ya mkusanyiko mkubwa, pasina hofu ya chochote wala kuhofia hatari wala kupiga mahesabu ya kukengeuka.

Ndugu zangu wapendwa, muitikio wenu kwa ufahamu wa kimakosa kuhusiana na Shari'ah leo na kuua kwenu kila wazo ambalo linaiharibu Dini yetu unaweza kumfanya Nabii wetu (saw) Siku ya Hukumu kusema atakapokuona: “Uso uliofaulu.” Kwa hiyo, wataka kuwa kama Abdullah bin Unays (ra)? Kuwa wa kwanza kwa maadui kifikra, kikauli na kivitendo kama alivyokuwa shujaa huyu.

Na wacha nikuulize swali muhimu: Lau ungelikuwa Mtume (saw), je yeye (saw) angekuchagua wewe katika misheni hiyo? Uwanja uko wazi, ndugu zangu, na maadui wa Uislamu ni wengi. Kwa hiyo, kuwa kama Abdullah bin Unays (ra) na jifunze kuunusuru Uislamu na uwe ngao yake kutokamana na hatari kama alivyofanya shujaa huyu.

بسم الله الرحمن الرحيم

# Abu Bakr As-Siddiq (ra)

**Abu Bakr As-Siddiq (ra) – Aqeedah ya Kisiasa na mfano wa kishujaa wa kuigwa**

Iko misimamo ambayo haisahihishi makosa ya watu binasfsi au makundi pekee. Ni misimamo ambayo Mwenyezi Mungu (swt) anasahihisha makosa ya Ummah wote. Misimamo, kupitia kwayo, Mwenyezi Mungu (swt) anaulinda Ummah kutokengeuka. Na hili ndilo dhihirisho lenyewe katika misimamo ya kishujaa inayoyazunguka maisha ya Abu Bakr As-Siddeeq (ra). Kwani, misimamo yake iliyokuwa imekuwa yenye sifa ya kifikra, utambuzi na ukomavu wa hali ya juu kwa kuwa ndio msingi na kanuni, na kuwa na ruwaza ya kisiasa na nyingine nyingi.

Msimamo wa kishujaa wa kwanza wa Abu Bakr (ra) ni ule aliochukua baada ya kifo cha Mtume (saw). Msimamo huu wa kishujaa unaonesha namna Abu Bakr (ra) alivyokuwa makini na mtambuzi juu ya suala la kiitikadi katika kuifahamu Dini ya Mwenyezi Mungu (swt). Pale Mtume (saw) alipofariki, watu wengi katika Wapenzi wake walighafilika kimawazo. Baadhi yao walisema: “Mtume (saw) alikuwa hajafa,” “Yeyote aliyesema mtume amefariki, nitamkata kichwa chake.” Hapa ndugu zangu Aqeedah ilitikisika kutokamana na nguvu za kuzidiwa na hisia.

As-Siddeeq (ra) aliweza kujizuia na kuwa makini kiutambuzi na kifikra, na kuziweka mbele kuliko hisia pale aliposema: “Yeyote aliyekuwa anamuabudu Muhammad (saw), basi ajue kwamba Muhammad (saw) amekufa. Na yeyote aliyekuwa anamuabudu Mwenyezi Mungu (swt) basi ajue kwamba Mwenyezi Mungu (swt) daima yuko hai na hafi.” Hakuna shaka kwamba Abu Bakr (ra) alikuwa ni mmoja katika Masahaba waliopendwa zaidi na Mtume (saw) na alikuwa wa mwanzo katika kujitoa muhanga kwa ajili Yake. Kwa masikitiko, kinyume na uwazi wa misimamo ya kishujaa kama hiyo, tunawaona watu leo wakitoa vijisababu vya kuwaruhusu watawala wanaowapenda kukengeuka, kwa hiyo wanayapa kipaumbele wanayofanya watawala badala ya kusonga mbele na kujifunga na Ahkam za Kishari’ah. Hivi sivyo Abu Bakr (ra) alivyokuwa. Bali, alisimama kidete na kuirudisha Aqeedah ya Kiislamu katika hali yake salama, hivyo basi mapenzi yake kwa Mtume (saw) yalikuwa ya kweli.

Msimamo wa pili wa shujaa, Abu Bakr (ra) ulikuwa kuwaelekea wale waliokataa kulipa Zaka. Msimamo wake wa kishujaa ulionekana kwa kuwa na msimamo na kutoruhusu kukubali kulegeza kamba katika kanuni, na katu kutoingia katika makubaliano juu ya jambo lolote pasina kuzingatia ni dogo kiasi gani, kukataa utekelezaji wa polepole wa Uislamu kiukamilifu. Msimamo wa Umar (ra) ulikuwa ni kama wa Masahaba wengine juu ya wale waliokataa kulipa Zaka, ambapo alisema: “Ewe Abu Bakr, utawapigaje vita watu ambao wanatamka shahada La ilaha illa Allah, Muhammad Rasool Allah?” Kwa hilo, ndugu zangu, Sayyiduna Abu Bakr (ra) alimshika ukosi na kusema: “Ewe Umar, wewe ni mwenye nguvu katika Ujahiliya lakini dhaifu ndani ya Uislamu? Haukumsikia Mtume (saw) akisema: “isipokuwa kile ambacho ni haki yake” na Zaka ni katika haki yake. Kwa jina la Mwenyezi Mungu, nitampiga vita yeyote anayetenganisha baina ya Sala na Zaka, kwa kuwa Zaka ni haki juu ya mali. Kwa jina la Mwenyezi Mungu (swt), lau hata watakataa kulipa kamba ambayo walikuwa wakilipa kwa Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw), nitawapiga vita kwa kukataa kwao kuilipa.” Kwa misimamo hii, ndugu zangu, Abu Bakr As-Siddeeq (ra) inatufundisha sisi kwamba hesabu za Dini hazipigwi kwa msingi wa faida na hasara. Bali, ni kwa msingi wa kujifunga na kuwa na msimamo thabiti. Alitambua kuipuza Zaka ni kuipunguza Dini. Moja katika mambo adhimu ya kuigwa ni pale Abu Bakr As-Siddeeq (ra) aliposema: “Dini haitopungua ilhali bado niko hai.” Twahitaji misimamo ya kishujaa mingi aina hii kutoka kwa mashujaa wetu wakubwa leo. Waislamu wengi, kwa masikitiko, wameridhia na kukubalia kulegeza misimamo na kukubali kutawaliwa na chengine kisichokuwa wahyi wa Mwenyezi Mungu (swt) na kugawanya madaraka na Makafiri. Yote haya, ndugu zangu ni kutokamana na makosa na utambuzi wa kimakosa ambao wahitaji misimamo ya kishujaa kuweza kuiondosha kutoka katika mabongo ya Waislamu ili waweze kurudi katika usafi na uwazi kama walivyokuwa Masahaba wa mwanzo.

Msimamo wa kishujaa mwengine wa Abu Bakr As-Siddeeq (ra) ni kwamba, msimamo wake mkubwa ni pale ambapo walioritadi ni wengi (Ridda). Kwa kuwa makabila ya Kiarabu yaliritadi kutoka Uislamu

***Endelea... UK 11***

baada ya kufariki Mtume (saw). Jeshi la Musailama Al-Kadhab lilikuwa na wapiganaji 40,000. Kwa maana nyingine, twaweza sema lau uchaguzi wa haki na uwazi ungelifanywa wakati huo, Abu Bakr (ra) asingeshinda. Kwa kuwa, watu wengi, wenye umaarufu na usemi hawakuwa upande wa Masahaba. Bali walikuwa Banu Hanifa, Musailama na wengine. Abu Bakr As-Siddeeq (ra) alipambana na hali hii vipi? Msimamo wake (ra) ulikuwa wa kipekee na wakishupavu. Alipigana vita dhidi ya Walioritadi kwa ukali pasina huruma, aliwatuma majenerali kuwapiga hadi pale alipowarudisha wakiwa wamesalimu amri chini ya nidhamu na Shari'ah ya Uislamu. Hii ilikuwa ni kutoka katika Tawfeeq ya Mwenyezi Mungu (swt) kwa Abu Bakr (ra) aliyeipa nguvu Dola ya Kiislamu na kutokiuka sheria zilizowekwa na nidhamu ya Uislamu. Moja katika natija ya vita hivyo vilivyopiganwa, ni kurudi kwa wengi katika Walioritadi katika twaa na utekelezaji wa sheria zote za Kiislamu. Kwa jina la Mwenyezi Mungu (swt), lau ingelikuwa sio kwa ujasiri wa msimamo wa Abu Bakr (ra), watu hawa wangelikuwa wenye ushawishi na nguvu ndani ya dola ya Kiislamu.

Msimamo mwengine mkubwa wa Abu Bakr (ra) ni kulituma jeshi la Usama hapa ndipo dhihirisho la sifa ya kishujaa ya kumuiga Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw) na kufuata maagizo yake. Tudhanie  ndugu zangu! Baada ya kufariki Mtume (saw), eneo lote lilikumbwa na wimbi la Ridda. Tudhanie pamoja, nchi iingie katika vita vya kindani vya kinyama ambavyo zaidi ya makundi 10 makubwa ya waasi wa kindani, wakiuana. Kisha kiongozi wa nchi hii anatuma jeshi, ambalo limeandaliwa ma kiongozi wa awali, kupigana na nchi jirani. Abu Bakr (ra) hakuwa akiitizama hali kwa mtizamo huu. Bali, msimamo wake ulikuwa ni kwamba Mtume (saw) alijuwa bora zaid, pale alipolituma jeshi la Usama. Kwa hiyo, angelisema: "Inawezekana vipi Nabii wa Mwenyezi Mungu (saw) amtume na kisha mimi nimsitishe?" Kwa hiyo akalituma jeshi la Usama kwa Warumi ilhali kulikuwa na makumi ya maelfu ya Walioritadi na walio epuka kutoa Zaka pembezoni mwa Madinah. Abu Bakr (ra) alikuwa anatambua hatari zote lakini alikuwa na Imani ya nguvu katika njia ya Mtume (saw). Jeshi la Usama likaondoka na hili liliwasababishia Warumi kuingiwa na hofu na Waarabu walipoteza ari ya kupigana walipofikiria kwamba haiwezikani kwa Abu Bakr kulituma jeshi hili ilhali Madinah ilikuwa haina ulinzi wa kutosha. Lakini uhalisia ulikuwa kwamba hakuna ulinzi. Lakini kulikuwa na yakini juu ya Mwenyezi Mungu (swt). Warumi wakakimbia, kwa hiyo jeshi la Usama halikupigana na kurudi na ushindi, kisha makabila ya Walioritadi wakashindwa, kwa hiyo yeye (ra) akaurudisha umoja na nguvu kwa Dola ya Kiislamu na mafunzo makubwa yapo kwa Abu Bakr (ra) kwa kutokubali kubezwa hata Hukm moja au agizo la Nabii (saw). Ni kwa kiwango gani tunahitaji viongozi, mashujaa na wenye misimamo kama hii. Twamuomba Mwenyezi Mungu (swt) atuwezeshe kushuhudia kwa pamoja misimamo kama hii ya kishujaa. Twamuomba Mwenyezi Mungu (swt), Mwenye Uwezo kuturudish tena kwenye misimamo iliyochukuliwa na mashujaa hawa. Yeye (swt) ndiye Bwana wetu mwenye uwezo wa hilo na ndiye wa kutegemewa.



بسم الله الرحمن الرحيم

# Muumini kutoka katika Familia ya Yaseen

**Kauli ya Kishujaa**

Ipo misimamo ambayo inafanana na shughuli za shahada; misimamo inayochukuliwa na watu binafsi kwa kuyapa kipaumbele maslahi na majukumu ya Da'wah kuliko maisha na maslahi yao. Moja katika misimamo ya kustaajabisha ni iliyotajwa katika Qur'an iliyochukuliwa na muumini kutoka katika familia ya Yaseen; mwanamume aliyeiamini Da'wah ya Mwenyezi Mungu (swt) na manabii, katika mji ambao watu wake walikuwa Makafiri wakosefu wa shukrani. Mwenyezi Mungu (swt) aliwatumia nabii mmoja baada ya mwengine; manabii watatu walikanwa na kutishiwa. Licha ya yote haya, na licha ya kuwa na maradhi makali na kuwa mbali, mwanamume huyu aliamua kucheza dori yake katika Da'wah na akaja kwa haraka kutoka mbali pembezoni mwa mji. "Akasema, "Enyi watu wangu, wafuateni manabii."" Kwa hiyo, walimkana, wakampiga na kumuua, kiasi kwamba akapata tunu ya Mwenyezi Mungu kumuonesha Jannah Siku ya Hukumu. "Alisema, "Natamani watu wangu wangelijua."

Ndugu zangu, tunaweza kupata funzo la kishujaa kutokamana na historia hii ya kishujaa. Moja katika haya ni twajifunza kuwa na huruma; huruma ambayo mbebaji Da'wah anatakiwa kuwa nayo kwa ajili ya Ummah wake. Pale mwanamume huyu alipoona ufisadi katika watu wake, hakuwakata, wala kusema "hakuna heri yoyote katika watu hawa" na kuanza kuwapiga viboko kama tunavyosikia siku hizi usiku na mchana: "sisi hatuna heri yoyote," "tumeshindwa," "Wamagharibi wameshinda." Bali huruma ilidhihirika ndani yake kama ilivyokuwa kwa Mtume wetu: "Ewe Bwana wangu, waongoze watu wangu, kwani hawajui."

Moja katika mafunzo ni kwamba wabebaji Da'wah ni lazima wasijitenge na Ummah kwa kutoa vijisababu kwamba tunajiweka sawa sisi kwanza. Da'wah ya kweli ni kujirekebisha binafsi na mujtama kwa wakati mmoja kama alivyofanya shujaa huyu; hakujitenga na kufuata shughuli zake za kujirekebisha binafsi. Bali aliwalingania watu wake.

Moja katika mafunzo ni kufanya haraka na sio kutoa udhuru. Aliwakimbilia kutoka mbali pembezoni mwa mji. Licha ya kuwa na kifafa, hakutoa udhuru na kusema "nyumba yangu iko mbali." Bali alikuja akiwakimbilia akiwa na matarajio yaliyojaa wasiwasi. Hakuna kama waliojitia hamnazo. Na hili, ndugu zangu, ndio kipimo kinacho watofautisha watu katika kuitikia Da'wah: "Ama kwa yule aliyekujia kwako akiwa anajitahidi" na "Na yule asiyejali kama ana mahitaji." Unatoka katika kambi ipi kati ya hizi mbili?

Moja katika mafunzo, ndugu zangu, ni kwamba Da'wah yahitaji kutekelezwa na sio tu kuiamini. Huyu mwanamume hakusema "nimeamini yaliyokuja na manabii." Hakusema "amininі." Bali, alisema "fuateni." "Alisema, "Enyi watu wangu, wafuateni manabii."" Kwa maana tekelezeni waliyokuja nayo. Na hilo ndilo tunalohitaji leo. Ni wangapi waliohifadhi Kitabu cha Mwenyezi Mungu. Tunachohitaji ni Kitabu cha Mwenyezi Mungu kutekelezwa na sheria zake zifuatwe ndani ya Dola na wenye mamlaka Ardhini.

Moja katika mafunzo, ndugu zangu, ni katazo la kukata tamaa na kuwaachia wengine. Huyu mwanamume aliwaona wabebaji Da'wah na Manabii wanakanwa na kutishiwa. Hakuingiwa na hofu. Hakukata tamaa. Hakuwaachia wengine na kusema "Ni kazi yao, mimi yanihusu nini ikiwa mitume wamefeli." Katu hakufanya hivyo. Bali, alicheza dori yake na kuwalingania kama ambaye yeye ndiye aliyetumwa. Hili ndilo tunalohitaji, ndugu zangu, kutoka kwa watoto na mabarobaro Waislamu leo. Lazima tuichukulie kauli "Amka na uonye" kama ambaye tumefunuliwa sisi. Hivi ndivyo Masahaba wa mwanzo walivyokuwa. Utukufu wa Da'wah, ndugu zangu, huhitaji kuwa na misimamo ya kishujaa ambayo Mwenyezi Mungu (swt) huibakisha milele na kuwanyanyua wanaotajwa katika wale walioichukua kama anavyo nyanyua kutajwa kwa waumini kutoka familia ya Yaseen. Kwa hiyo, yeyote anayetaka Mwenyezi Mungu (swt) kunyanyua utajo wake, basi afanye haraka kuchukua nafasi yake miongoni mwa wabebaji Da'wah leo na labda tutanyanyuliwa (huko Akhera) pamoja na waliotangulia na Mwenyezi Mungu (swt) hunyanyua utajo wetu katika 'Illiyyun. Yeye (swt) ndiye Bwana wetu mwenye uwezo wa hilo na ndiye wa kutegemewa.

بسم الله الرحمن الرحيم

# HudHud - Da'wah ya Kisiasa ya Kimataifa

Shujaa wa simulizi yetu yaa leo sio mtume, wala Sahaba, wala mwanamume au mwanamke mwema. Je, utaamini kuwa msimamo wa kishujaa uliochukuliwa katika kisa hiki leo ulikuwa sio wa mwanadamu? Ndugu zangu, zipo safu za Majini yamesimama, wanyama na ndege, wote wanamsubiri mfalme. Mfalme anawasili na kukagua safu. Anapokagua safu ya ndege, anasema: “Kwa nini simuoni hudhud – au ni miongoni mwa ambao hawakuhudhuria? Hakika, nitamuadhibu kwa adhabu kali au nitamchinja isipokuwa anipe sababu yenye kuingia akilini.” Amekwenda wapi huyu HudHud – HudHud wa Sayyiduna Sulayman (as) – ilhali akijuwa umuhimu wa kuondoka katika safu? Kulikuwa na kitu katika akili ya HudHud ambacho kilikuwa kinamkosesha utulivu. Alipaa juu ya Palestina, akiwacha ufalme uliostawi ambao hautapewa mwengine yeyote na pia una Dini kwa kuwa mfalme wake ni Mtume wa Mwenyezi Mungu (swt). Yote haya hayakumfanya kuwa mzembe na kubweteka na kuishi nyumbani kibinafsi. Bali alijituma juu zaidi ya Palestina na kupaa Bara Arabu kote kutoka upande hadi upande, akisafiri maelfu ya maili. Kisha kwa haraka alirudi na ripoti kamili. “Lakini yeye [kwa maana HudHud] hakuchukua muda mrefu” akawa mbele ya Sulayman (as). Tukio ambalo lingewatia hofu Majini. Alisema: “Nimepata maarifa ambayo kwamba wewe huna, na nimekuja kutoka Sheba (huko Yemen) na habari fulani. Hakika, nimempata mwanamke anawatawala, na amepewa kila kitu, na ana kiti cha enzi kizuri.” Alikasirishwa sana; inawezekanaje kuwepo kiti cha enzi kinachotawala kwa kisichokuwa wahyi wa Mwenyezi Mungu (swt). Kisha akaendelea kama ambaye analaumu kuhusu tatizo lake binafsi: “Kwa hiyo hawasujudu kwa Mwenyezi Mungu (swt), ambaye anayafichua yaliyofichika ndani ya mbingu na ardhi na anajua unayoyaficha na unayoyadhihirisha – Mwenyezi Mungu (swt) – hakuna mungu isipokuwa Yeye, Bwana wa Kiti Kitukufu cha Enzi.” Alitaja mara mbili “kiti kitukufu cha enzi” katika ripoti yake kama ambaye alimtaka Sayyiduna Sulayman kuchukua hatua na asikubali uwepo wa ardhi au kiti cha enzi katika dunia kinacho hukumu kinyume na wahyi wa Mwenyezi Mungu (swt). Kwa haraka, ndugu zangu, Sayyiduna Sulayman (as) alipokea ripoti, alighairisha adhabu na akampandisha cheo mwanajeshi huyu kuwa balozi. “Chukua hii barua yangu na wafikishie. Kisha wawache na uone [jibu] wakalolirudisha.” HudHud aliondoka kwa safari hiyo tena iliyokuwa imezungukwa na hatari na mashaka. HudHud aliondoka lakini Sayyidsuna Sulayman (as) alikuwa na wasiwasi. Yeye (as) alikuwa amesikia kwamba kuna kiti cha enzi chengine ambacho kinahukumu kinyume na wahyi wa Mwenyezi Mungu (swt). Yeye (as) aliwatizama waliokuwepo naye na akasema: “Nani kati yenu ataniletea kiti chake cha enzi kabla hawajanijia wakiwa wamesalimu amri?” “Mmoja mwenye nguvu miongoni mwa Majini alisema, “Mimi nitakileta kama huja nyanyuka kutoka sehemu yako”” Kwa hiyo takribani kama baada ya saa moja. Sayyiduna Sulayman (as) hakukubali na hakuridhika na hilo na alikitaka haraka zaidi. “Akasema mmoja aliyekuwa na maarifa kutoka katika Kitabu, “Mimi nitakileta kabla hujapesa.” Na alipokiona [Suleyman] kimewekwa mbele yake, alisema, “Hii ni katika fadhila za Bwana wangu”” Sasa, ndugu zangu, Sayyiduna Sulayman (as) hakuweza kupumzika. Na ni matukio machache baadaye ambapo Malkia wa Sheba, aliyekuwa akiabudu jua, alikuwa mlangoni mwa kasri la Sulayman (as) akiingia huku akisema: “Bwana wangu, nimejikosea, na nasalimu amari kwa Mwenyezi Mungu wa Sulayman, Bwana wa ulimwengu.”

Nani shujaa katika hadithi hii? Nani shujaa katika tukio hili? Ni HudHud aliyetukuzwa, mbebaji Da’wah wa kimataifa. Ndugu zangu, twajifunza kutoka kwa kisa cha HudHud wa Sayyiduna Sulayman (as) kwamba mbebaji Da’wah hatakiwi kujifunga kwa ajili ya kujibadilisha binafsi. Bali, hutakiwa kwenda mbio kujibadilisha, kuibadilisha jamii na dola. Sio kujifunga na mambo ya Da’wah ya kibinafsi ya kiroho ambayo wengi katika watu wanatulingania kwa masikitiko. Twajifunza kuhusu Da’wah ya siasa ya kimataifa ili kuleta watu wote na ardhi zote chini ya Uislamu. Twajifunza kwamba kutawala kinyume na wahyi wa Mwenyezi Mungu (swt) na kufanyakazi ili kuondosha viti au mamlaka juu ya ardhi lazima liwe ndio lengo la kila Muislamu anayemuamini Mwenyezi Mungu (swt). Twajifunza kuhusu ushikamano wa mtawala na anaowatawala juu ya ujumbe mmoja. Hivi ndivyo ilivyokuwa na kumfanya HudHud kutokuwa na uoga. Yeye (as) alijuwa kwamba mtawala na mtawaliwa lazima washirikiane kueneza ujumbe mmoja na Da’wah moja duniani kote. Ndugu zangu, kuna viti vingapi leo ambavyo vinatawala kinyume na wahyi wa Mwenyezi Mungu (swt)? Ni nchi ngapi zilizopo ambazo hazimsujudii Mwenyezi Mungu (swt) katika sheria na tungo zao? Mwenyezi Mungu (swt) aliporekodi hichi kisa katika Qur’an, Anakuambia wewe na mimi tuwe na misimamo kama ya HudHud na tuwe na ari kubwa kama alivyokuwa yeye. Kwa hiyo, je, tunao walio na ghera ya kufanyakazi ya siasa ya kimataifa na Da’wah ya kiitikadi ili kuweza kuileta dunia [katika Uislamu] na kuviangusha viti vyote chini ambavyo havihukumu na yale ambayo yamefunuliwa na Mwenyezi Mungu (swt).

بسم الله الرحمن الرحيم

# Wachawi wa Fir'awn
# Ushujaa wa kurudi katika haki

Lau kukubali haki ndio utukufu basi kujitoa muhanga kwa ajili ya ukweli ni ushujaa. Hususan pale ambapo msimamo huu unamaanisha kukataa yakini, maslahi na ufuasi ambao mtu alikuwa ameushikilia maishani mwake. Katika kisa hiki, hakuna tu shujaa mmoja. Bali kuna kundi la mashujaa. Wote walichukua misimamo ya kishujaa: Wachawi wa Fir'awn. Walikuwa mfano wa vyombo vya habari ambavyo vilipigia debe uongo wake, kuuficha ukatili wake, na kujadiliana na wanaompinga kwa niaba yake. Walikuwa wasaidizi wake na waliomnusuru na ambao ssdori yao ilikuwa kudhibiti rai ya ummah ili kumuunga mkono Fir'awn. Fir'awm aliposhindwa mbele za Sayyiduna Musa (as) na kuona miujiza ya mkono na fimbo, alihisi kiti chake kimetikiswa. Fir'awn akaagiza miongoni mwa waliokusanyika mjini.

Wako wapi wadanganyifu? Wako wapi waliobobea katika kucheza na akili za watu? Wako wapi wachawi ambao wako makini katika kuficha vitu na mambo? Wachawi walikusanywa. Wachawi walihitaji nini baada ya kufanya mazingaombwe yao? Wachawi walikuja kwa Fir'awn na kusema, "Hakika, tupewe zawadi lau tutashinda." Akasema, "Sawa, na [zaidi ya hayo], mutakuwa miongoni mwa walioko karibu [nami]." "Mutateuliwa katika vyeo muhimu ndani ya serikali na mutaungwa mkono na kiongozi wa serikali."

Mchuano ukaanza. Wachawi wakatupa vijidude vyao na kuyahadaa macho ya watu kama ilivyo kawaida yao na kuwakinaisha watu kwamba vijikamba vyao vinatembea. Hata Musa (as) akahisi uoga kutokamana na yale ambayo yeye (as) aliyaona katika ukafiri wao. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu (swt) akamtia nguvu: Mwenyezi Mngu (swt) alisema,

**[قُلْنَا لَا تَخَفْ إِنَّكَ أَنتَ الْأَعْلَىٰ]**

**"Usikhofu! Hakika, wewe ndiye utakaye shinda."** [20. Taha: 68]

**[وَأَلْقِ مَا فِي يَمِينِكَ تَلْقَفْ مَا صَنَعُوا ۖ إِنَّمَا صَنَعُوا كَيْدُ سَاحِرٍ ۖ وَلَا يُفْلِحُ السَّاحِرُ حَيْثُ أَتَىٰ]**

**"Na kitupe kilicho katika mkono wako wa kulia; kitavimeza walivyo viunda. Hakika, walivyo unda ni hila za mchawi tu, na mchawi hafanikiwi popote afikapo."** [20. Taha: 69]

Wachawi waliona [nyoka] ya kweli iliyovimeza vijidude vyao na kumshinda mtawala waliyekuwa wanamuhudumikia. Ni upi msimamo wao baada ya kushindwa? Hapa, kaka na dada zangu ndio kilele cha ushujaa wao. Labda wachawi wote walijuwa kuwa kumpinga Fir'awn hakukumaanisha tu kifo, bali kukatwa mikono yao, miguu yao na kusulubiwa katika magogo ya mitende. Licha ya yote haya, ushujaa wao ulisonga mbele: **"Amua utakavyoamua. Waweza kuamua katika haya maisha ya duniani."** Wachawi walidondoka chini na kusujudu. Walisema, **"Tumemuamini Bwana wa Harun na Musa."**

Kaka zangu, twawaambia wasaidizi wa makatili leo: Enyi wasaidizi wa makatili, ima ni wanahabari, asasi za usalama, wanachuoni waovu na wengineo… munaweza kuwa sio wabaya kupitiliza kama wachawi wa Fir'awn walivyokuwa kabla kuamini, kwa hiyo, kwa nini musiwe kama wao baada ya kuamini. Kaka na dada zangu, jifunze kwamba hata ikawa mtu amezama katika ukafiri na kuiuza nafsi yake kwa shetani, anaweza kubadilisha hali yake juu chini kwa mpigo mmoja uliokuwa na ikhlasi na kurudi haraka upesi katika haki. Hii ikiwa kwa Mwenyezi Mungu (swt) ni ushujaa. Twajifunza kwamba haizingatiwi ni ukafiri kiasi gani na ni kiwango gani cha rai ya ummah kimepotoshwa, kwa msimamo mmoja wa kishujaa, watu watabadilika na kuwafuata wabebaji Da'wah kama msimamo wa Banu Isra'eel ulivyobadilika na kumfuata Sayyiduna Musa (as) baada ya kuona msimamo wa wachawi.

**Enyi Waislamu,** Wamagahribi na wasaidizi wao leo wanatuonyesha uchawi mbele ya macho yetu na kututupia mawazo yao na kutufanya tudhanie kupitia uchawi wao, kwamba ustaarabu wao ndio uliosahihi, wenye heri na unaoleta furaha kwa watu. Wametupa mbele zetu mawazao ya kuthamini vitu, uhuru, demokrasia, usekula nk, wakiwashtua watu kupitia hayo. Wametuletea uongo uliovuka mipaka. Ummah ulisimama na kuhisi hofu ndani yake kutokana na nguvu za ukafiri na kusahau kwamba unabeba miujiza ambayo, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu (swt), ni mikubwa kuliko hata miujiza ya fimbo ya Musa (as) na iliyo na sumu zaidi kuliko vijikamba na uhadaifu wa Ukafiri.

Hivyo basi, Enyi Waislamu, musiwe na hofu. Hakika, nyinyi ndio washindi. Tupeni yaliyomo katika mkono wenu wa kulia. Iwekeni mbele Qur'an kama mbadala wa ukafiri. Kwa jina la Mwenyezi Mungu (swt), itavimeza vyote vilivyobuniwa. Na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu (swt), tutashuhudia siku ambapo wachawi wote watadondoka chini wakisujudu, kwa kujisalimisha, na wakiwa watumwa kwa sheria za Mwenyezi Mungu (swt), Bwana wa ulimwengu.

# Mashujaa kutoka katika Kisa cha Ndovu

سُورَةُ الفِيلِ

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

أَلَمْ تَرَ كَيْفَ فَعَلَ رَبُّكَ بِأَصْحَٰبِ ٱلْفِيلِ ١ أَلَمْ يَجْعَلْ كَيْدَهُمْ
فِى تَضْلِيلٍ ٢ وَأَرْسَلَ عَلَيْهِمْ طَيْرًا أَبَابِيلَ ٣ تَرْمِيهِم
بِحِجَارَةٍ مِّن سِجِّيلٍ ٤ فَجَعَلَهُمْ كَعَصْفٍ مَّأْكُولٍۭ ٥

Wakati mwingine misimamo ya kisaliti huonekana sawia na misimamo ya kishujaa katika tukio moja. Hivyo kunaonekana dunia mbili tofauti kati yao. Katika kisa cha ndovu, wako wanaume mashujaa pamoja na wasaliti waovu. Ni kufananaje huku kwa zama zao na zetu! Abraha Al-Ashram alikuwa ni mfalme wa Abyssinia aliyetaka kuwavutia Waarabu ambao alikuwa akiwaonea wivu kwa majivuno ya maadili yao na Ka'bah. Kwa hiyo, alijenga kanisa kubwa la Qullays na kuwasiliana na mkubwa wake, Najashi (Negus) ili kupata uungwaji mkono kwa ujenzi wa kanisa kubwa kwa ajili ya Wakristo. Ama kuhusu Waarabu, hawakulipa umuhimu Qullays au kuvutiwa na mapambo yake. Haswa, Muarabu mwanaume kutoka Kinanah alimfunza Abraha somo ambalo hatolisahau: alisafiri kutoka huko kote hadi kwenye Qullays, akajisaidia, kisha akazipaka kuta zake uchafu wa Muarabu huyo. Abraha alipoziona kuta zilivyo fanywa akaamua kwenda kuiteka na kuivunja Ka'bah. Jeshi likaanza safari. Kisha ikaanza misimamo ya kishujaa. Mwanamume Muarabu akiitwa “Dhu Nafar,” aliwakusanya wale wote alioweza  kuwakusanya na kuwa nao: “Abraha analenga kusambaratisha mwenendo wenu wa maisha, mustakbali wenu, Nyumba Tukufu ya Mwenyezi Mungu.” Wakakabiliana naye lakini walishindwa na Dhu Nafar akachukuliwa mateka. Akasonga mbele na kukabiliwa na shujaa mwengine kutoka katika kabila la Khath'am ambaye alifanya kitu kama hicho kwa kuwakusanya watu kunusuru na kukabiliana na Abraha lakini aliwashinda na kumchukua kiongozi wao mateka, ambaye jina lake ni “Nufayl bin Habeeb.” Alipofika Taif. Alifikiria kwamba “Bait Al-Laat” iliyoko Taif ndio Ka'bah na alitaka kuibomoa na hapa, ndugu zangu, ikaanza misimamo ya kisaliti. Msaliti kutoka Thaqeef akiitwa “Mas'ood Ath-Thaqafi” alimwambia Abraha hii sio Ka'bah, Nyumba Tukufu ya Mwenyezi Mungu iko njia ile. Akamuonyesha pale ilipokuwa Ka'bah ya Mwenyezi Mungu na kumtuma huko akifuatana na kibaraka mkubwa miongoni mwa Waarabu ili kuwaongoza: “Abu Rughal.” Walipokuwa njiani, kabla kuifikia Ka'bah, Abu Rughal alifariki na kuzikwa. Kaburi lake lilipigwa mawe kwa miongo baadaye kama ishara ya usaliti kwa Waarabu. Kisha, ndugu zangu, Abraha aliwasili na kumsukuma ndovu “Mahmoud” kusonga mbele kuivunja Ka'bah. Lakini Nufayl bin Habeeb alipita mbele na kulishika sikio la ndovu na kulipigia kelele: “Mahmoud, kaa chini au rudi ukiwa na tahadhari; uko katika Nyumba Tukufu ya Mwenyezi Mungu. Ndugu zangu, ndovu alikaa chini, na hakutekeleza agizo. Mwenyezi Mungu alishukisha miujiza ya makundi ya ndege ambayo yaliliangamiza jeshi la Abraha.

Ndugu zangu, Wamagharibi ni muungano dhidi yetu, na wanatufikiria mchana na usiku. Wanauonea wivu Ummah wetu kwa sababu ni msafi na uliotunukiwa Dini ambayo wote wanataabika kwa kuwa mbali nayo. “Hata wale ambao hawakuamini miongoni mwa Watu wa Kitabu [kwa maana Mayahudi na Wakristo] wala washirikina wanatamani tusipate

*Endelea... UK 16*

heri yoyote isitufikie kutoka kwa Bwana wenu." Wanakwenda mbio kututoa katika Dini kwa kuipamba kwa ustaarabu wao kama Abraha alivyoipamba Qullays. Wanatuona tunamiliki kile ambacho hawana: utulivu wa kiroho, kiungo cha familia, hadhi ya wanawake, utukufu wa sheria za Kiislamu, namna Uislamu unavyosafisha mali, unavyopangilia ghariza, unavyolinda mujtama kutokamana na ulafi na uchu wa vitu ambao unayaangamiza maisha yao. Wanayaona yote haya ilhali upande mwingine wanaona kuwa wana: familia zilizovunjika, upweke, kujitoa uhai, maradhi na viwango vikubwa vya uhalifu. Yote haya yanawakasirisha kwa hiyo wanajaribu kuwahadaa Waislamu kuhusu yale waliyo nayo. Wanaupamba ustaarabu wao kuwa ni wa kisayansi, maendeleo, ustawi na ubora wa maisha.

Ndugu yangu Muislamu, jifunze kutoka kwa Muarabu wa Kinanah usipumbazwe na mapambo na upuzi wa Wamagharibi. Iamini Dini yako na kiweke kichwa chako makini na jivunie ulichokuwa nacho. Fanyakazi uufichue uchafu wa ustaarabu wa Kimagharibi kama alivyofanya Muarabu wa Kinanah alivyoichafua Qullays. Jifunze kutoka kwa Dhu Nafar na Nufayl bin Habeeb na kuunusuru Ummah wako na sio kuogopa idadi ya Wamagharibi na majeshi yao. Wazindue Waislamu ili wasusie na walete mabadiliko pasina kukata tamaa au kuzembea na Mwenyezi Mungu atakuwa nawe na kuwasahilishia changamoto kwa idhini Yake. Lau mnyama (ndovu) alikataa kushirikiana na jamii ya kimataifa katika kuupiga vita Uislamu, kisha kwa jina la Mwenyezi Mungu, kila Muislamu anayeshirikiana na Wamagharibi leo, au watawala wao na kuwasaidia, anaridhia na kupigia debe fahamu zao ameporomoka chini ya wanyama na twahofia wanaweza kuletwa Siku ya Hukumu wakiwa pamoja na Abraha, Mas'ood Ath-Thaqafi na Abu Rughal, Kwa idhini ya Mwenyezi Mungu, Ummah utawachukulia hatua wasaliti miongoni mwa Waarabu na wasiokuwa Waarabu, na kuyapiga mawe majina yao kama wanavyofanya Waarabu kaburi la Abu Rughal. Bora katika yale tunayojifunza kutoka katika kisa cha ndovu ni kwamba pasina kuzingatia nguvu za Ukafiri utakavyokuwa, hatimaye ushindi ni kwa wenye Taqwa. Kama ilivyokuwa kwa Mwenyezi Mungu kulituma kundi la ndege pale ambapo babu yake Nabii (saw) alipokuwa hana hata kundi la kukabiliana na Abraha, kisha sisi wafuasi wa Nabii (saw), twamuomba Mwenyezi Mungu atufanye sisi ndio kundi la ndege ambalo litauangamiza Ukafiri, na kuufanya kama majani yaliyoliwa kwa idhini ya Mwenyezi Mungu (swt).